**OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**

# HOTUBA YA MHE. HAMZA SAIDI JOHARI, MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI KATIKA SHEREHE YA 71 YA KUWAKUBALI NA KUWAPOKEA MAWAKILI WAPYA 524

**VIWANJA VYA KARIMJEE, DAR ES SALAAM**
**12 DISEMBA, 2024**

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

- **Mheshimiwa Prof. Ibrahim Hamis Juma, Jaji Mkuu wa Tanzania;**
- **Waheshimiwa Majaji wa Mahakama ya Rufani Tanzania;**
- **Mhe. Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi, Mahakama Kuu ya Tanzania;**
- **Waheshimiwa Majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania;**
- **Prof. Sist Joseph Mramba, Mkuu wa Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania;**
- **Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Elimu ya Sheria;**
- **Mheshimiwa Eva Nkya, Msajili Mkuu wa Mahakama;**
- **Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama;**
- **Mheshimiwa George Herbert, Msajili wa Mahakama ya Rufani,**
- **Bw. Sylvester Anthony Mwakitalu, Mkurugenzi wa Mashtaka;**
- **Dkt. Ally Possi, Wakili Mkuu wa Serikali;**
- **Wakili Boniphace Anyisile Kajunjumele Mwabukusi, Rais wa Chama cha Mawakili wa Kujitegemea (TLS);**
- **Waheshimiwa Mabalozi na Wawakilishi wa Taasisi na Mashirika ya Kimataifa;**

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

- **Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama wa sasa na Wastaafu mliopo;**
- **Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa na Dini mliopo;**
- **Waheshimiwa Wasajili na Naibu Wasajili;**
- **Waheshimiwa Mahakimu;**
- **Watendaji na Watumishi wa Mahakama mliopo;**
- **Mawakili wa Serikali na Mawakili wa Kujitegemea;**
- **Mawakili wote wapya pamoja na ndugu Wazazi, Walezi, jamaa na marafiki waliowasindikiza siku ya leo;**
- **Ndugu wanahabari;**
- **Wageni waalikwa;**
- **Mabibi na Mabwana.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**Mheshimiwa Jaji Mkuu;**

Awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa yote kwa kutukutanisha siku hii ya leo kwenye sherehe ya 71 ya kuwapokea na kuwakubali Mawakili wapya 524.

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

Ninakushukuru wewe binafsi Jaji Mkuu na uongozi mzima wa Mahakama kwa kunialika ili nitoe salamu za pongezi kwa Mawakili wapya wanaokubaliwa na kupokelewa siku ya leo. Kwa niaba ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, napenda kuwapongeza kwa dhati kabisa mawakili wapya mliokubaliwa leo kuingia katika orodha ya Mawakili Tanzania. ***Hongereni sana!***

**Mheshimiwa Jaji Mkuu;**

Nitumie nafasi hii kuipongeza Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo (The Law School of Tanzania) kwa kazi kubwa ya kuwaandaa Mawakili hawa. Hatua waliyofikia ni matokeo ya jitihada za muda mrefu si tu kwa Mawakili wenyewe bali pia hata kwa wale waliowasaidia kufikia hatua hii ikiwemo walimu waliowafundisha, wazazi, walezi Serikali, waajiri na wadau mbalimbali waliowalipia ada za masomo ama kuwapatia fursa za kupata mafunzo mbalimbali ya kuwanoa. Kwa ujumla nawashukuru na kuwapongeza wote.

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

**Mheshimiwa Jaji Mkuu;**

Ikiwa ni mara yangu ya kwanza kusimama katika hadhara hii tokea nilipoteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, nitumie fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini na kuniteua kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na mshauri mkuu katika masuala yote ya kisheria nchini. Aidha, natoa shukrani za dhati kwa Serikali ya awamu ya sita kwa kutoa kipaumbele cha kuendeleza sekta ya sheria nchini. Nafarijika sana ninapoona Mawakili hawa wakiongezeka hapa nchini kwetu mwaka hadi mwaka kwa kiasi kikubwa. Ni imani yangu kuwa, ongezeko hili la Mawakili litakuwa na mchango mkubwa wa kuondoa changamoto mbalimbali za kisheria nchini na Ofisi yangu itakuwa bega kwa bega kufanikisha azma ya Serikali yetu ya awamu ya sita ya kuboresha mfumo wa haki jinai na haki madai.

**Mheshimiwa Jaji Mkuu;**

Nitumie nafasi hii kutoa pole kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na kuungana na watanzania wenzangu kuwaombea wenzetu waliopoteza

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

maisha kwa kuangukiwa na jengo, eneo la Kariakoo jijini Dar es Salaam. Aidha, kwa niaba ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali natoa pole kwa Mahakama na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuondokewa na viongozi waliohudumu katika nyadhifa mbalimbali hivi karibuni. Mwenyezi Mungu azipumzishe roho zao mahali pema peponi. Amina.

**Mheshimiwa Jaji Mkuu;**

Pamoja na salamu za Pongezi kwa Mawakili waliokubaliwa na kupokelewa leo, naomba nitumie siku hii adhimu kuwaeleza Mawakili wapya kuwa, wana nafasi kubwa sana ya kuondoa changamoto mbalimbali za kisheria katika Taifa hili. Nafahamu kuwa jukumu hilo hawawezi kulitekeleza peke yao bila kuishirikisha Serikali na wadau mbalimbali wa utoaji haki nchini. Mawakili ni wahusika muhimu katika kudumisha ustawi wa sheria. Hakuna nafasi ya kufanya maamuzi yanayokiuka haki za binadamu au matumizi mabaya ya mamlaka. Kila hatua mnapochukua inapaswa kuzingatia haki, uwazi, na usawa. Hivyo, nitaeleza kwa kifupi namna ambavyo Mawakili wa

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

Kujitegemea wanaweza kuisaidia Serikali kupunguza au kuondoa kero za wananchi katika maeneo mbalimbali nchini.

**Mheshimiwa Jaji Mkuu;**

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inatambua mchango mkubwa wa Mahakama katika jukumu la utoaji haki nchini ikiwa ni utekelezaji wa Ibara ya 107A (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika kutekeleza wajibu huo, Mawakili ni kiungo muhimu sana baina ya wananchi na Mahakama katika kuichambua na kuitafsiri haki na sheria. Nitumie nafasi hii kuwaeleza Mawakili mliokubaliwa leo kuwa, mna nafasi kubwa katika kuhakikisha jukumu la utoaji haki linatekelezwa kwa ufanisi na Mahakama. Kama Maafisa wa Mahakama mnapaswa kuhakikisha mnaisadia Mahakama kutekeleza jukumu la utoaji haki nchini kwa kutoa tafsiri sahihi za sheria ili kuisaidia Mahakama itende haki na kuhakikisha wananchi wanapatiwa haki zao wanapokwenda Mahakamani au kwenye vyombo vingine vya kisheria, sio tu pale kesi inapokuwa inaendelea hata wakati wa utekelezaji wa hukumu. Katika harakati zenu za kusimamia haki, ni muhimu kujua kuwa jukumu lenu ni kubwa zaidi ya kuwawakilisha

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

wateja. Ninyi ni walinzi wa haki, wawakilishi wa uadilifu, na watetezi wa sheria katika jamii yetu. Hivyo basi, napenda kusisitiza mambo muhimu ambayo lazima mzingatie kama sehemu ya maadili ya kitaaluma ya sheria. Ni imani yangu kuwa, mkitimiza wajibu wenu kikamilifu malalamiko ya wananchi kuhusu kutotendewa haki yatapungua kwa kiasi kikubwa.

Katika hotuba ya Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliyoitoa mwaka 1985 katika Chuo Kikuu cha Jawaharial Nehru kilichopo New Delhi nchini India, alisema, nanukuu:

> ***"… if we fail to establish Constitutions and laws which allow people to struggle peacefully towards greater justice, then ultimately, after all other methods have failed, they will break those laws in search for justice."***

Kwa tafsiri isiyo rasmi ya maneno hayo:

> ***"endapo tutashindwa kuwa na Katiba na Sheria ambayo inaruhusu watu kupigania haki zao kwa amani, hatimaye, njia nyingine zote zikishindikana, watavunja sheria ili wapate haki zao".***

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

Nukuu hiyo inawataka mfahamu nafasi yenu kama Mawakili kuwa jukumu lenu la msingi ni kuhakikisha sheria zinasaidia kutafuta haki. Sambamba na hilo, ni wajibu wetu sote Mawakili kuhakikisha wananchi wanapatiwa haki zao kwa wakati.

**Mheshimiwa Jaji Mkuu;**

Natambua na kuiunga mkono Serikali yetu na taasisi mbalimbali zinazotoa huduma za msaada wa kisheria nchini. Mawakili wote ikiwa ni pamoja na Mawakili mlioapishwa siku ya leo mnapaswa kushiriki katika Wiki ya Sheria na Kampeni mbalimbali za kutoa misaada ya kisheria na kutoa elimu ya sheria kwa wananchi katika maeneo mbalimbali nchini.

Mwaka 2023 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilianzisha Kamati za Ushauri wa Kisheria katika ngazi za Mikoa na Wilaya ili kurahisha ufikiwaji wa huduma za ushauri wa kisheria kwa wananchi. Miongoni mwa majukumu ya Kamati hizo ni kusaidia wananchi kupata haki zao mahali ambako haki hizo zinaweza kupatikana ili kupunguza malalamiko ya wananchi dhidi ya Serikali na kulazimika kutembea umbali mrefu kutafuta haki zao.

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

Ni vema tukishirikiana kuwaeleza wananchi kuhusu uwepo wa Kamati hizo ili baadhi ya kero ziwe zinatatuliwa katika ngazi za mikoa na Wilaya. Tunapoelekea uchaguzi mkuu, niwaombe mkawe mabalozi wa kutoa elimu kuhusu sheria za uchaguzi kupitia vyombo mbalimbali vya habari ili kujenga uelewa chanya kwa wananchi.

**Mheshimiwa Jaji Mkuu;**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 hadi 2023/2024 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilipanga kuboresha utoaji huduma za kisheria kwa lengo la kukabiliana na mabadiliko ya kimazingira, kiuchumi, kibiashara na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Katika kufanikisha lengo hilo, Miswada **75** ya Sheria iliandaliwa ambapo kati ya hiyo, Miswada **63** ilipitishwa Bungeni na kuwa sheria za nchi; Sheria **858** (Sheria Kuu na Sheria Ndogo) zimetafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili; Sheria **1,604** (Sheria Kuu na Sheria Ndogo) zimefanyiwa urekebu; na Sheria Ndogo **5,020** ziliandaliwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Sheria ndogo hizo zimehakikiwa na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali na kuanza kutumika. Sheria hizi zinajumuisha Kanuni, Matangazo, Amri na Matamko ya Serikali.

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

Kwa kuwa zoezi la uandaaji wa mapendekezo ya kutunga au kurekebisha sheria, kutafsiri au kufanya urekebu ni endelevu, ni rai yangu kwenu Mawakili wapya kuhakikisha mnatoa maoni ambayo yatasaidia kutunga sheria ambazo zitakuwa na tija kwa Taifa letu. Tarehe 1 Novemba, 2024 Baraza la Uongozi la Chama cha Mawakili Tanganyika (Tanganyika Law Society – TLS) lilinitembelea Ofisini kwangu na niliwaeleza kuwa TLS ni miongoni mwa wadau muhimu wanaoishauri Serikali kuhusiana na utekelezaji wa Sheria mbalimbali nchini. Kwa kuwa Mawakili mliokubaliwa leo ni wanachama wa TLS, ni muhimu tuendelee kudumisha uhusiano huo kwa maslahi ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Jaji Mkuu;**

Kama mjumbe wa Kamati ya Maadili ya Mawakili wa Kujitegemea, nawasihi Mawakili wote mliokubaliwa na kupokelewa leo muwe na nidhamu si tu mnapokuwa mahakamani bali hata mnapokuwa katika jamii inayotuzunguka. Kwa kuwa nimebaini bado kuna changamoto ya uwepo wa Mawakili wa Kujitegemea ambao hawana nidhamu na hawazingatii Kanuni za Maadili ya taaluma ya sheria, nitumie fursa hii kuwaahidi

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

kwamba, nitaendelea kudhibiti nidhamu za Mawakili wa Kujitegemea kwa kuzingatia mamlaka niliyopewa kupitia Sheria ya Mawakili, Sura ya 341.

Nitumie fursa hii kuwaeleza kuwa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imepokea maboresho yaliyoletwa kuhusiana na taratibu za kushughulikia nidhamu za Mawakili wa Kujitegemea na inaendelea kuyafanyia kazi kwa kushirikiana na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa tunazalisha Mawakili wenye nidhamu na weledi wa hali ya juu. Pia ni jukumu la TLS kuendelea kusisitiza mara kwa mara kwa wanachama wake umuhimu wa kuzingatia misingi ya uaminifu, uadilifu na taaluma zao katika kazi zao za kila siku.

**Mheshimiwa Jaji Mkuu;**

Sote tunafahamu usemi unaosema *"elimu haina mwisho"*. Nawasihi Mawakili mliokubaliwa na kupokelewa leo kuendelea kujiendeleza kielimu na kujifunza kwa watangulizi wetu waliotangulia ambao wanaofanya vizuri. Katika ulimwengu huu wa sasa, Mawakili wanapaswa kuendana na mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, kimazingira na kiteknolojia. Hivyo, tunapaswa kusoma fani mbalimbali na sio sheria tu. Hii itasaidia kujenga uelewa mpana katika maeneo mbalimbali ya kisheria.

HOTUBA YA MWANASHERIA

Hivi sasa kuna miradi mingi ya kimkakati nchini ambayo inatarajiwa kuanza kutekelezwa na mingine inaendelea kutekelezwa. Miongoni mwa miradi hiyo inahitaji umakini mkubwa wa kuandaa nyaraka mbalimbali za kisheria ikiwemo mikataba. Serikali itahitaji kupata maoni yenu kama wadau ili kuhakikisha miradi hiyo italeta tija na kuzingatia maslahi mapana ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Jaji Mkuu;**

Ujumbe wangu wa leo kwa Mawakili waliokubaliwa na kupokelewa ni kwamba: ***"Msiogope kufanya kitendo au vitendo ambavyo mnaamini ni sahihi wakati mnapotekeleza majukumu yenu ya uwakili"***. Nendeni mkazungumze kwa niaba ya wale ambao hawawezi kuzungumza wenyewe ***(Be the voice of those who cannot speak for themselves***). Matendo unayofanya ndio yanayokuweka tofauti, hivyo unapaswa kuamua ni aina gani ya tofauti unayotaka kuifanya ***(What you do makes a difference and you have to decide what kind of difference you want to make).***

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

**Mheshimiwa Jaji Mkuu,**

Kabla sijahitimisha hotuba yangu, naomba nimalizie kwa kuwakumbusha ujumbe uliotolewa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, tarehe 9 Disemba 2024 wakati wa kuadhimisha miaka 63 ya Uhuru wa Nchi yetu. Katika ujumbe huo alisisitiza watanzania tujivunie na kwa pamoja tuendelee kufanya kazi ya kuzilinda na kuzitunza tunu za amani, umoja na mshikamano ambazo ndizo nguzo za mafanikio yetu. Ni imani yangu kuwa Mawakili mliokubaliwa leo na wote tuliofika hapa siku ya leo tutaendelea kuzienzi tunu hizo na kutekeleza majukumu yetu kwa kuzingatia sheria na maelekezo mbalimbali yaliyotolewa na viongozi mbalimbali wa nchi yetu siku ya Uhuru ili kuendelea kudumisha amani, umoja na ushirikiano nchini.

**Mheshimiwa Jaji Mkuu;**

Baada ya kusema hayo naomba sasa nimalize hotuba yangu kwa kuwatakia kila la kheri Mawakili wote 524 waliokubaliwa na kupokelewa siku ya leo. Nafahamu kwamba kuna wengine wengi ambao nao wanatamani sana kuwa Mawakili lakini bado hawajafanikiwa.

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

Nawaomba wasikate tamaa hata kidogo bali waendelee kujitahidi hadi nao waweze kufikia hatua hii. Nimalizie kwa kutoa tena shukrani zangu za dhati kwako Mheshimiwa Jaji Mkuu kwa kunialika siku ya leo. Nimefurahi sana kujumuika pamoja nanyi.

**NAWATAKIA HERI YA MWAKA MPYA WA 2025**

**AHSANTENI SANA**

Hamza S. Johari
**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**
12 Disemba, 2024

HOTUBA YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI